

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

<b>Simu ya mdomo:</b>	027 - 29 77402
<b>Tel Fax:</b>	027- 29 77402
<b>E-mail:</b>	<i>handenidc@yahoo.com</i>
<b>Kumb. yako :</b>	
<b>Kumbu yetu :</b>	HW/S.20/96/5



**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (H/W)  
S.L.P. 355,  
Handeni, Tanga,  
Tanzania**

02/08/2017

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni amepokea kibali cha ajira Kumb. CFC.26/205/01'FF'/99 cha tarehe 22 Agosti, 2017 na kibali Kumb.Na. FA. 170/369/01/69 cha tarehe 14 Agosti, 2017 kuajiri nafasi mbalimbali Thelathini na saba (37) kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kupitia kibali hicho, anawatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa zinazohitajika kuomba kujaza nafasi wazi nne (4) za Mtendaji wa Kijiji (3), Dereva (1). Aidha, nafasi 35 zilizobaki zitatangazwa na kushughulikiwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa mujibu wa taratibu. Hivyo basi, Halmashauri ya Wilaya Handeni inatangaza nafasi za Udereva na Mtendaji wa Kijiji kama ifuatavyo:-

**1/ DEREVA DARAJA LA II (Nafasi 1)**

**A. Sifa, Elimu na Ujuzi**

Mwombaji awe amehitimu na kufaulu mihani wa kidato cha nne mwenye leseni Daraja C ya urndeshaji na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila rekodi ya kusababisha ajali, mwenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la Pili (Trade Test Certificate Grade II)

**B. Ngazi ya Mshahara**

Cheo cha Dereva II kina ngazi ya mshahara **TGOS A.**

**C. Majukumu/Kazi za Dereva II**

- i/ Kuendesha magari ya abiria na malori.
- ii/ Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote, na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari.
- iii/ Kufanya matengenezo madogo katika gari.
- iv/ Kuandika na kutunza daftari la safari (log book) kwa kila safari.

**2/ MTENDAJI WA KIJIKI III (Nafasi 3)**

**A. Sifa, Elimu na Ujuzi**

Mwombaji awe na elimu ya kidato cha nne au cha sita na kuhitimu Astashahada/cheti katika fani Utawala, Sheria, Fedha, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi ya Jamii kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali.

**B. Ngazi ya Mshahara**

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji III kina ngazi ya mshahara TGS B

**C. Kazi/Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji III**

- i/ Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya.
- ii/ Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
- iii/ Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji;
- vii/ Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
- v/ Katibu wa Mkikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;
- vi/ Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
- vii/ Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
- viii/ Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji;
- ix/ Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji;
- x/ Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji;
- xi/ Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ZOTE**

- i/ Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii/ Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na kutumwa kwenye anwani ilitajwa hapo chini.
- iii/ Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa. Maelezo binafsi (CV) na nyaraka zote muhimu pamoja na picha 2 (passport size) zilizopigwa hivi karibuni.
- iv/ Kwa wale watakaopitwa kwenye mchujo wa awali (Short listed candidates) ndio watakaoitwa kufika kwenye usaili (Interview) na kufika na vyeti halisi.
- v/ Nafasi ya kazi aliyoomba iandikwe juu ya bahasha, kutozingatia hili kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili.
- vi/ Barua zote za maombi zitumwe kwa anwani ifuatayo;

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI,  
S. L. P 355,  
HANDENI.**

Aidha, uwasilishaji wa barua za maombi kwa mkono katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya hazitapokelewa.

**Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ni tarehe 11 Septemba, 2017.**

.....  
William M. Makufwe  
**Mkurugenzi Mtendaji (H/W)**  
**HANDENI.**

Nakala: Mbao zote za matangazo.  
Halmashauri ya Wilaya  
**Handeni.**